**JINA_____________________________________________ DAR___________ NAMBARI_________**

# TEACHER.CO.KE

**102/3**

**KISWAHILI KIDATO CHA NNE**

**FASIHI**

**Karatasi ya 3**

**Muda**: **Saa 2½**

**TERM 1 2022**

ALAMA

**Maagizo**

- Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- Jibu maswali **manne** pekee.
- Swali la **kwanza** ni la **lazima**.
- Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani: Riwaya, Ushairi na Tamthilia.
- Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja**.
- Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| **Sehemu** | **A** | **B** | | **C** | | **D** | | **JUMLA** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Swali** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** | **6** | **7** | |
| **Alama** | | | | | | | | |

## SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI

**Lazima.**

1. Hapo zamani za kale paliishi sungura na ndovu. Wanyama hawa waliishi baharini.Maulana alikuwa amewatunukia mapenzi si haba.Makazi yao yalikuwa yamepambwa yakapambika.Walitegemea matunda mbalimbali yaliyokuwa baharini kama mapera, matomoko matikitimaji na kadhalika.

Siku moja usiku wa manane, maji yakaanza kupwa.Ndovu aliathirika zaidi. Alijaribu kuinama majini lakini hakuweza . Alimwita sungura amsaidie lakini sungura alikuwa ametoweka. Ndovu aliamua kwenda kumtafuta sungura. Alimtafuta hadi msituni lakini hakumpata. Alihofia kurudi baharini na hadi wa leo yumo msituni.

**Maswali**

a)Tambua utanzu na kijipera chake. (al.2)

b)Taja fomyula zingine **mbili** za kutanguliza kifungu hiki. (al.2)

c)Eleza umuhimu wa kijipera hiki. (al.5)

d)Eleza sifa za kifungu hiki. (al.5)

e)Eleza umuhimu wa fomyula:

(i)Kutanguliza (al.3)

(ii)Kuhitimisha (al.3)

## SEHEMU B: TAMTHILIA

**Pauline Kea:** *Kigogo*

***2. "Kubali pendekezo letu la kufungwa kwa soko… huoni hii ni fursa nzuri ya kulipiza kisasi? Najua umekuwa ukimmezea mate…''***

(a) Fafanua muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(b) Bainisha vipengele viwili vya kimtindo katika dondoo hili. (alama 4)

(c) Kufungwa kwa soko ni ukatili. Mbali na ukatili huu, toa mifano mingine ya ukatili kwenye tamthilia. (alama 6)

(d) Msemaji wa maneno haya ni mshauri mbaya. Thibitisha kauli hiyo kwa kurejelea mifano yoyote sita katika tamthilia ya *Kigogo* (alama 6)

***Au***

**3.** "Wananchi katika mataifa ya Afrika wanakumbwa na tatizo la uongozi mbaya." Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa mujibu wa Tamthilia. **(alama 20)**

## *SEHEMU YA C: RIWAYA*
## *Assumpta K. Matei: Chozi la Heri*

4. Kipi kinachowavuta raia kuhamia ughaibuni? Angeuliza nafsi yake pale ambapo mzigo wa simanzi na ukiwa ulipokilemea kifua chake. Je, ni huo mshahara mnono unaowageuza kuwa watumwa wa kufanya kazi kidindia ati kwa kudai kuwa nchi za ughaibuni ni twenty-four-hour economies?

a. Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)
b. Huku ukitolea mifano maridhawa, fafanua mbinu nne za kimtindo zinazojitikeza katika dondoo hili (Alama 4)

c. Eleza changamoto inayomkumba msemaji katika dondoo hili. (Alama 2)
d. Fafanua jinsi maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili yameshughulikiwa kwingineko riwayani. (Alama 4)
e. Fafanua umuhimu wa mandhari katika kuijenga riwaya hii kwa kurejelea Msitu wa Mamba (Alama 8)

***Au***

5. Eleza jinsi **maudhui ya ufisadi** yalivyoshughulikiwa katika riwaya ya **Chozi la Heri.** (al 20)

## SEHEMU D: USHAIRI

6. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

**KAMA SODOMA!**

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Haihitaji makini, kwa mwenye macho mazima
Utaona walakini, mradi ukitizama
Wanazini hadharani, wana kwa watu wazima
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Wanazini hadharani, wana kwa watu wazima
Wanatafuna maini, vijana na kina mama
Hawana haya nyusoni, wameharamisha wema
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Hawana haya nyusoni, wameharamisha wema
Baba na binti ndani, wanacheza lelemama
Marijali wa mbioni, kujipagaza umama
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Marijali wa mbioni, kujipagaza umama
Wameikataa dini, toka tumboni mwa mama
Wadai Wataliani, watajirisha mapema
Yafanana na sodoma, mji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Wadai ufirauni, watajirisha mapema
Hivyo mambo ya kigeni, yametunukiwa dhima
Uwaonapo fuoni, nusu uchi wa mnyama
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Uwaonapo fuoni, nusu uchi wa mnyama
Watu hawana imani, umezidi uhasama
Na viongozi wa dini, kuabudu darahima
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama sodoma!
Na viongozi wa dini, kuabudu darahima
Wamekeuka yamini, kati yao na Rahima
Wamemuasi Manani, na kusahau kiyama
Yafanana na sodoma, miji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Wamemuasi manani, na kusahau kiyama
Ya Illahi tuauni, tuwe watu maamuma
Tukue katika dini, siku zetu za uzima
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini.

**Maswali**

(a) Bainisha bahari ya shairi hili ukijikita katika ruwaza zifuatazo (alama3)
- i) Mishororo
- ii) Maneno
- iii) Vina

(b) Eleza muundo wa shairi hili (alama4)

(c) Bainisha mbinu zifuatazo za kimtindo katika shairi hili (alama3)
- i) Tashbihi
- ii) Taswira
- iii) Tasfida

(d) Eleza toni ya shairi hili (alama1)

(e) Bainisha nafsi nenewa katika shairi hili (alama1)

(f) Fafanua dhamira ya mtunzi wa shairi hili (alama2)

(g) Andika ubeti watatu kwa lugha tutumbi (alama4)

(h) Fafanua maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa na mshairi (alama2)
- i) Manani
- **ii)** Marijali

***Au***

***7.*** **Soma *shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

Maendeleo ya umma
Sio vitu maghalani
Kama tele vimesaki
Lakini havishikiki
Ama havikamatiki
Bei juu

Maendeleo ya umma
Sio vitu gulioni
Kuviona madukani
Kuvishika  mikononi
Na huku wavitamani
Kama tama ya fisi
Kuvipata ng'o

Maendeleo ya umma
Sio vitu shubakani
Dhiki ni kwa mafakiri
Nafuu kwa mafakiri
Ni wao tu washitiri
Huo ni uistimari
Lo! Warudia

Maendeleo ya umma
Ni vitu kumilikiwa
Na wanyonge kupatiwa
Kwa bei kuzingatiwa
Bila ya kudhulumiwa
Na hata kuhadaiwa
Hiyo ni haki.

Maendeleo ya umma
Dola kudhibiti vitu
Vijapo nchini mwetu
Na kuwauzia watu
Toka nguo na sapatu
Pasibakishiwe na kitu
Huo usawa.

Maendeleo ya umma
Watu kuwa na kauli
Katika zao shughuli
Vikaoni kujadili
Na mwisho kuyakubali
Maamuzi halali
Udikteta la.

Maendeleo ya umma
Watu kuwa waungwana
Vijakazi na watwana
Nchini kuwa hakuna
Wote kuheshimiana
Wazee hata vijana.

**Maswali**

a) Eleza dhamira ya shairi hili. (al.2)
b) Baininsha tamathali mbili za usemi katika shairi hili. (al.2)
c) Eleza umuhimu wa usambamba katika shairi hili. (al.2)
d) Onyesha jinsi maendeleo ya umma yalivyo kinaya. (al.2)
e) Eleza mambo ambayo mshairi anachukulia kuwa maendelo halisi ya umma. (al.4)
f) Tambua matumizi ya mistari mishata kwa kutolea mifano. (al.2)
g) Bainisha nafsi neni katika shairi hili. (al.1)
h) Fafanua toni ya shairi hili. (al.1)
i) Andika ubeti wa nne kwa lugha nathari. (al.4)

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA**

***Kila la Heri!!***